Scriptures taken from Kiswahili Contemporary Version
Copyright (c) 1984, 1989, 2006 by International Bible Society(R)
Used by permission. All rights reserved worldwide.

NOTE: 141 quotations of The Word 2014 in Kiswahili have not been formatted yet.
Please contact hs2013 at bible2.net to format the quotations
conveniently in your browser.

Taken from The Holy Bible, English Standard Version
copyright (c) 2001 by Crossway Bibles,
a division of Good News Publishers.
Used by permission. All rights reserved.

# Neno Februari 2014
# The Word February 2014

Kiswahili Contemporary Version 2006
English Standard Version

Project Bible 2.0 www.bible2.net

## Neno la Jumapili, 2. Februari 2014

*Yesu akawaambia Mitume:*
Vivyo hivyo nanyi mkiisha kufanya mliyoagizwa, semeni,
"Sisi tu watumishi tusiostahili,
tumefanya tu yale tuliyopaswa kufanya."
*Luka 17,10*

*Yohana akasema:*
Yeye hana budi kuwa mkuu
zaidi na mimi nizidi kuwa mdogo.
*Yohana 3,30*

*Jesus said to the apostles:*
So you also, when you have done all
that you were commanded, say,
We are unworthy servants;
we have only done what was our duty.
*Luke 17:10 (ESV)*

*John said:*
He must increase, but I must decrease.
*John 3:30 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 27. Februari 2014

Lakini wewe,
Ee BWANA, usiwe mbali, Ee Nguvu yangu, uje haraka unisaidie.
*Zaburi 22,19*

Ilipofika saa tisa Yesu akapaza sauti akalia,
“Eloi, Eloi lama sabakthani?”
Maana yake, “Mungu wangu,
Mungu wangu, mbona umeniacha?”
*Mathayo 27,46*

---

You, O Lord, do not be far off!
O you my help, come quickly to my aid!
*Psalm 22:19*

About the ninth hour Jesus cried out with a loud voice,
saying, Eli, Eli, lema sabachthani?
that is, My God, my God, why have you forsaken me?
*Matthew 27:46 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 4. Februari 2014

Nayainua macho yangu nitazame vilima,
msaada wangu utatoka wapi?
Msaada wangu hutoka kwa BWANA,
Muumba wa mbingu na dunia.
*Zaburi 121,1-2*

Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote,
kwa maana hakuna Jina jingine
chini ya mbingu walilopewa
wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.
*Matendo ya Mitume 4,12*

---

I lift up my eyes to the hills.
From where does my help come?
My help comes from the Lord,
who made heaven and earth.
*Psalm 121:1-2 (ESV)*

There is salvation in no one else,
for there is no other name under heaven given among men
by which we must be saved.
*Acts 4:12 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 25. Februari 2014

Usimhukumu mtumishi wako,
kwa kuwa hakuna mtu anayeishi mwenye haki mbele zako.
*Zaburi 143,2*

Sitashika hasira yangu milele.
Ungama dhambi zako tu kwamba umemwasi BWANA Mungu wako.
*Yeremia 3,12-13*

---

Enter not into judgment with your servant,
for no one living is righteous before you.
*Psalm 143:2 (ESV)*

I am merciful, declares the Lord;
I will not be angry forever.
Only acknowledge your guilt,
that you rebelled against the Lord your God.
*Jeremiah 3:12-13 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 6. Februari 2014

Nuru huangaza wenye haki na furaha
kwa watu wanyofu wa moyo.
*Zaburi 97,11*

Hata gizani nuru humzukia mtu mwadilifu,
yule mwenye rehema, huruma na haki.
*Zaburi 112,4*

---

Light is sown for the righteous,
and joy for the upright in heart.
*Psalm 97:11*

Light dawns in the darkness for the upright;
he is gracious, merciful, and righteous.
*Psalm 112:4*

## Neno la Jumapili, 23. Februari 2014

Ukuu na uweza, Ee BWANA, ufalme ni wako,
umetukuzwa kuwa mkuu juu ya yote.
*1 Mambo ya Nyakati 29,11*

Ufalme wako uje.
Mapenzi yako yafanyike hapa
duniani kama huko mbinguni.
*Mathayo 6,10*

---

Yours is the kingdom, O Lord,
and you are exalted as head above all.
*1 Chronicles 29:11 (ESV)*

Your kingdom come,
your will be done,
on earth as it is in heaven.
*Matthew 6:10 (ESV)*

## Neno la Jumamosi, 8. Februari 2014

Waheshimuni na kuwatanguliza wengine.
*Warumi 12,10*

Msitende jambo lo lote kwa nia ya kujitukuza,
bali kwa unyenyekevu,
kila mtu akimhesabu mwingine bora kuliko nafsi yake.
*Wafilipi 2,3*

---

Outdo one another in showing honor.
*Romans 12:10 (ESV)*

Do nothing from rivalry or conceit,
but in humility count others more significant than yourselves.
*Philippians 2:3 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 21. Februari 2014

Alipoona makutano aliwahurumia
kwa sababu walikuwa wanasumbuka na bila msaada,
kama kondoo wasio na mchungaji.
*Mathayo 9,36*

*Kristo asema:*
Mimi ndimi Mchungaji Mwema:
Ninawajua kondoo Wangu nao kondoo Wangu wananijua.
*Yohana 10,14*

---

When Jesus saw the crowds,
he had compassion for them,
because they were harassed and helpless,
like sheep without a shepherd.
*Matthew 9:36 (ESV)*

*Christ says:*
I am the good shepherd.
I know my own and my own know me.
*John 10:14 (ESV)*

## Neno la Jumatatu, 10. Februari 2014

Lakini walivyozidi kuteswa
ndivyo walivyozidi kuongezeka na kuenea katika nchi,
Wamisri wakawaogopa Waisraeli,
*Kutoka 1,12*

Wingi wa watu ni utukufu wa mfalme,
bali pasipo watu mkuu huangamia.
*Mithali 14,28*

---

The more they were oppressed,
the more they multiplied and the more they spread abroad.
And the Egyptians were in dread of the people of Israel.
*Exodus 1:12*

In a multitude of people is the glory of a king,
but without people a prince is ruined.
*Proverbs 14:28*

## Neno la Jumatano, 19. Februari 2014

Wote wakutafutao na washangilie na kukufurahia,
wale wapendao wokovu wako daima na waseme,
“Mungu na atukuzwe!”
*Zaburi 70,4*

Je, Mungu hakuwachagua wale walio maskini
machoni pa ulimwengu kuwa matajiri katika imani
na kuurithi Ufalme aliowaahidi wale wampendao?
*Yakobo 2,5*

---

May all who seek you rejoice
and be glad in you!
May those who love your salvation
say evermore, “God is great!”
*Psalm 70:4 (ESV)*

Has not God chosen those who are poor in the world
to be rich in faith and heirs of the kingdom,
which he has promised to those who love him?
*James 2:5 (ESV)*

## Neno la Jumatano, 12. Februari 2014

Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote,
ila ni Mungu Mwana pekee,
aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha.
*Yohana 1,18*

*Yohana aeleza kuhusu mji takatifu mbinguni:*
Usiku hautakuwako tena,
wala hawatahitaji mwanga wa taa au wa jua,
kwa maana Bwana Mungu atakuwa nuru yao,
nao watatawala milele na milele.
*Ufunuo wa Yohana 22,5*

---

No one has ever seen God;
the only God, who is at the Father's side,
he has made him known.
*John 1:18 (ESV)*

*John describes the heavenly city:*
Night will be no more.
They will need no light of lamp or sun,
for the Lord God will be their light,
and they will reign forever and ever.
*Revelation 22:5 (ESV)*

## Neno la Jumatatu, 17. Februari 2014

Kila bonde litajazwa, kila mlima na kilima kitasawazishwa.
Njia zilizopinda zitanyooshwa,
zilizoparuza zitasawazishwa.
*Luka 3,5*

Nikiwa pamoja na Mungu wangu nitaweza kuruka ukuta.
*Zaburi 18,29*

---

Every valley shall be filled,
and every mountain and hill shall be made low,
and the crooked shall become straight,
and the rough places shall become level ways.
*Luke 3:5 (ESV)*

By my God I can leap over a wall.
*Psalm 18:29 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 14. Februari 2014

Kwako Bwana mataifa yatakujia kutoka
miisho ya dunia na kusema,
"Baba zetu hawakuwa na cho c
hote zaidi ya miungu ya uongo,
sanamu zisizofaa kitu ambazo hazikuwafaidia lo lote."
*Yeremia 16,19*

Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopagawa na pepo,
naye akawatoa wale pepo kwa neno lake,
na kuponya wagonjwa wote.
*Mathayo 8,16*

---

To you shall the nations come
from the ends of the earth and say:
Our fathers have inherited nothing but lies,
worthless things in which there is no profit.
*Jeremiah 16:19 (ESV)*

That evening they brought to Jesus
many who were oppressed by demons,
and he cast out the spirits with a word
and healed all who were sick.
*Matthew 8:16*

## Neno la Jumamosi, 1. Februari 2014

Wenye busara wamelikataa neno la BWANA,
hiyo busara waliyo nayo ni ya namna gani?
*Yeremia 8,9*

Fuateni upendo na kutaka sana karama za roho,
hasa karama ya unabii.
*1 Wakorinto 14,1*

---

The wise men have rejected the word of the Lord,
so what wisdom is in them?
*Jeremiah 8:9 (ESV)*

Pursue love, and earnestly desire the spiritual gifts,
especially that you may prophesy.
*1 Corinthians 14:1*

## Neno la Jumatatu, 3. Februari 2014

Kwa Mungu peke yake nafsi yangu inapata pumziko,
wokovu wangu watoka kwake.
*Zaburi 62,1*

Leo katika mji wa Daudi kwa ajili yenu amezaliwa Mwokozi,
ndiye Kristo Bwana.
*Luka 2,11*

---

For God alone my soul waits in silence;
from him comes my salvation.
*Psalm 62:1 (ESV)*

*The angel said to the shepherds:*
Unto you is born this day in the city of David a Savior,
who is Christ the Lord.
*Luke 2:11*

## Neno la Ijumaa, 28. Februari 2014

Tupe msaada dhidi ya adui,
kwa maana msaada wa mwanadamu haufai.
*Zaburi 60,11*

Yesu akawajibu,
"Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa."
*Luka 5,31*

---

Oh, grant us help against the foe,
for vain is the salvation of man!
*Psalm 60:11 (ESV)*

Jesus answered the Pharisees and their scribes,
Those who are well have no need of a physician,
but those who are sick.
*Luke 5:31 (ESV)*

## Neno la Jumatano, 5. Februari 2014

Nitakusifu Wewe, katikati ya mataifa,
nitaimba kuhusu Wewe katikati ya mataifa.
*Zaburi 57,9*

Ni vema kumshukuru BWANA na kuliimbia jina lako,
Ee Uliye Juu sana, kutangaza upendo wako asubuhi,
uaminifu wako wakati wa usiku.
*Zaburi 92,1-2*

---

I will give thanks to you, O Lord, among the peoples;
I will sing praises to you among the nations.
*Psalm 57:9 (ESV)*

It is good to give thanks to the Lord,
to sing praises to your name, O Most High;
to declare your steadfast love in the morning,
and your faithfulness by night.
*Psalm 92:1-2 (ESV)*

## Neno la Jumatano, 26. Februari 2014

Ee BWANA, usiniache, usiwe mbali nami,
Ee Mungu wangu.
*Zaburi 38,21*

*Yesu akasema:*
Lakini hata kama nikihukumu,
hukumu zangu ni sahihi kwa sababu sitoi hukumu yangu,
bali Mimi pamoja na Baba aliyenituma.
*Yohana 8,16*

---

Do not forsake me, O Lord!
O my God, be not far from me!
*Psalm 38:21 (ESV)*

*Jesus said:*
Even if I do judge, my judgment is true,
for it is not I alone who judge,
but I and the Father who sent me.
*John 8:16 (ESV)*

## Neno la Ijumaa, 7. Februari 2014

*Paulo akamwambia Elima (yule mchawi):*
Nawe sasa sikiliza, mkono wa Bwana u dhidi yako.
Utakuwa kipofu, wala hutaona jua kwa muda.
Mara ukungu na giza vikamfunika,
naye akaenda huko na huko akitafuta
mtu wa kumshika mkono ili amwonyeshe njia.
*Matendo ya Mitume 13,11*

Wapenzi, msiamini kila roho,
bali zijaribuni hizo roho mwone
kama zimetoka kwa Mungu,
kwa sababu manabii wengi wa uongo
wametokea ulimwenguni.
*1 Yohana 4,1*

---

*Paul said to Elymas the magician:*
“Behold, the hand of the Lord is upon you,
and you will be blind and unable to see the sun for a time.”
Immediately mist and darkness fell upon him,
and he went about seeking people to lead him by the hand.
*Acts 13:11 (ESV)*

Beloved, do not believe every spirit,
but test the spirits to see whether they are from God,
for many false prophets have gone out into the world.
*1 John 4:1 (ESV)*

## Neno la Jumatatu, 24. Februari 2014

Binadamu wa ngazi ya chini ni kama pumzi,
wa ngazi ya juu ni uongo,
wakipimwa kwenye mizani, si cho chote.
*Zaburi 62,9*

Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa ufufuo wa wafu.
Ule mwili wa kuharibika uliopandwa
utafufuliwa usioharibika.
*1 Wakorinto 15,42*

---

Those of low estate are but a breath;
those of high estate are a delusion;
in the balances they go up;
they are together lighter than a breath.
*Psalm 62:9 (ESV)*

What is sown is perishable;
what is raised is imperishable.
*1 Corinthians 15:42 (ESV)*

## Neno la Jumapili, 9. Februari 2014

BWANA akajibu,
“Uso wangu utakwenda pamoja nawe,
nami nitakupa raha.”
*Kutoka 33,14*

*Yesu asema:*
Njooni kwangu,
ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo,
nami nitawapumzisha.
*Mathayo 11,28*

---

The Lord said,
My presence will go with you,
and I will give you rest.
*Exodus 33:14 (ESV)*

*Jesus says:*
Come to me,
all who labor and are heavy laden,
and I will give you rest.
*Matthew 11:28 (ESV)*

## Neno la Jumamosi, 22. Februari 2014

Ee BWANA Mwenye Nguvu, ni nani aliye kama Wewe?
Ee BWANA, Wewe ni mwenye nguvu,
na uaminifu wako unakuzunguka.
*Zaburi 89,8*

Umenizunguka nyuma na mbele,
umeweka mkono wako juu yangu.
*Zaburi 139,5*

---

O Lord God of hosts,
who is mighty as you are, O Lord,
with your faithfulness all around you?
*Psalm 89:8 (ESV)*

You hem me in, behind and before,
and lay your hand upon me.
*Psalm 139:5 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 11. Februari 2014

Kiongozi wao atakuwa mmoja wao,
mtawala wao atainuka miongoni mwao.
Nitamleta karibu nami naye atanikaribia mimi,
kwa maana ni nani yule atakayejitolea kuwa karibu nami?’
asema BWANA.
*Yeremia 30,21*

Kristo ni mjumbe wa agano jipya,
ili kwamba wale walioitwa waweze
kupokea ile ahadi ya urithi wa milele,
Yeye alikufa awe ukombozi wao
kutoka katika dhambi walizozitenda
chini ya agano la kwanza.
*Waebrania 9,15*

---

*The Lord said to Israel and Judah:*
Their prince shall be one of themselves;
their ruler shall come out from their midst;
I will make him draw near, and he shall approach me.
*Jeremiah 30:21*

Christ is the mediator of a new covenant,
so that those who are called
may receive the promised eternal inheritance,
since a death has occurred that redeems them
from the transgressions committed under the first covenant.
*Hebrews 9:15 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 20. Februari 2014

Kwake kuna nguvu na ushindi,
adanganywaye na adanganyaye
wote wawili ni wake.
*Ayubu 12,16*

*Nebukadneza akasema:*
Nikamsifu Yeye Aliye Juu Sana,
nikamheshimu na kumhimidi Yeye aishiye milele.
Utawala wake ni utawala wa milele,
ufalme wake hudumu kizazi na kizazi.
*Danieli 4,34*

---

With God are strength and sound wisdom;
the deceived and the deceiver are his.
*Job 12:16 (ESV)*

*Nebuchadnezzar said:*
I blessed the Most High,
and praised and honored him who lives forever,
for his dominion is an everlasting dominion,
and his kingdom endures from generation to generation.
*Daniel 4:34 (ESV)*

## Neno la Alhamisi, 13. Februari 2014

Inuka na utusaidie, utukomboe kwa sababu
ya upendo wako usio na mwisho.
*Zaburi 44,26*

Bwana ataniokoa katika kila shambulio baya na kunileta
salama katika Ufalme Wake wa mbinguni.
Atukuzwe Yeye milele na milele.
*2 Timotheo 4,18*

---

Rise up; come to our help!
Redeem us for the sake of your steadfast love!
*Psalm 44:26 (ESV)*

The Lord will rescue me from every evil deed
and bring me safely into his heavenly kingdom.
To him be the glory forever and ever.
*2 Timothy 4:18 (ESV)*

## Neno la Jumanne, 18. Februari 2014

Wengi wanasema juu yangu," Mungu hatamwokoa.
Lakini wewe, Ee BWANA, ni ngao pande zote,
umeniwekea utukufu na kuinua kichwa changu."
*Zaburi 3,2-3*

Akasema, “Ee mtu upendwaye sana,
usiogope. Amani iwe kwako!
Uwe na nguvu sasa, uwe na nguvu.”
Alipozungumza nami, nilipata nguvu nikasema,
“Nena, bwana wangu, kwa kuwa umenipa nguvu.
*Danieli 10,19*

---

Many are saying of my soul,
there is no salvation for him in God.
But you, O Lord, are a shield about me,
my glory, and the lifter of my head.
*Psalm 3:2-3*

O man greatly loved,
fear not, peace be with you;
be strong and of good courage.
*Daniel 10:19*

## Neno la Jumamosi, 15. Februari 2014

Ee nafsi yangu kwa nini unasononeka?
Kwa nini unafadhaika hivyo ndani yangu?
Weka tumaini lako kwa Mungu,
kwa sababu bado nitamsifu,
aliye afya ya uso wangu Mwokozi
wangu na Mungu wangu.
*Zaburi 42,5*

Yule mgonjwa akamjibu,
“Bwana, mimi sina mtu wa kuniingiza bwawani maji
yanapotibuliwa.
Nami ninapotaka kutumbukia bwawani,
mtu mwingine huingia kabla yangu.”
Yesu akamwambia,
“Simama, chukua mkeka wako na uende.”
*Yohana 5,7-8*

---

Why are you cast down, O my soul,
and why are you in turmoil within me?
Hope in God;
for I shall again praise him, my salvation.
*Psalm 42:5 (ESV)*

The sick man answered Jesus,
Sir, I have no one
to put me into the pool when the water is stirred up,
and while I am going another steps down before me.
Jesus said to him,
Get up, take up your bed, and walk.
*John 5:7-8 (ESV)*

## Neno la Jumapili, 16. Februari 2014

BWANA Mwenye Nguvu yu pamoja nasi,
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.
*Zaburi 46,7*

Yeye peke yake ndiye mwamba na wokovu wangu,
ndiye ngome yangu, sitatikisika.
*Zaburi 62,6*

---

The Lord of hosts is with us;
the God of Jacob is our fortress.
*Psalm 46:7 (ESV)*

God only is my rock and my salvation,
my fortress; I shall not be shaken.
*Psalm 62:6 (ESV)*